# SHEKINAH THEOLOGICAL SEMINARY

# MWONGOZO WA CHUO

# (PROSPECTUS)

**Cheti & Diploma katika Theolojia**
**Programu ya Miaka Mitatu**

**Haki Miliki © 2025 Shekinah Theological Seminary (STS)**
**Haki Zote Zimehifadhiwa**

Hakuna sehemu yoyote ya chapisho hili inayoweza kunakiliwa, kutolewa tena, kuhifadhiwa katika mfumo wa kurejelea, au kusambazwa kwa njia yoyote ile—iwe kwa njia ya kielektroniki, kimitambo, kwa kupiga nakala, kurekodi, au kwa mbinu nyingine yoyote—bila ruhusa ya maandishi iliyoidhinishwa rasmi na Shekinah Theological Seminary (STS). Hii inahusu maandiko, picha, michoro, na nyenzo nyingine zote zilizomo katika chapisho hili.

**Anuani Rasmi:**
Shekinah Theological Seminary (STS)
S.L.P. 32807
45 Barabara ya Mivumoni, Mtaa wa Mivumoni
14130 Wazo, Kinondoni
Dar es Salaam, Tanzania

**Mawasiliano:**
Barua pepe: ststanzania2025@gmail.com
Simu: +255 759 883 388

**Toleo:**
Toleo la Kwanza – Agosti 2025
Imekusanywa na kuchapishwa Dar es Salaam, Tanzania

Prospectus hii imetolewa kwa madhumuni ya kutoa taarifa ya jumla kuhusu Shekinah Theological Seminary (STS), kozi zake, ratiba, sera na huduma zake. Hati hii haihusishi mkataba wa kisheria kati ya Chuo na mtu binafsi au taasisi yoyote, isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo kwa maandishi.

Shekinah Theological Seminary (STS) inahifadhi haki ya kufanya marekebisho, kuongeza, kubadilisha, au kuondoa maudhui yoyote yaliyomo katika hati hii bila kutoa taarifa ya awali. Wanafunzi na wadau wanashauriwa kuhakikisha wanapata taarifa za hivi karibuni moja kwa moja kutoka ofisi ya Chuo kabla ya kufanya maamuzi yoyote muhimu yanayohusiana na masomo au huduma zinazotolewa.

**UTANGULIZI**

Shekinah Theological Seminary (STS) ni taasisi ya Kikristo inayojibainisha kwa kutoa elimu ya Theolojia na malezi ya kiroho kwa wanaume na wanawake walio na wito wa kumtumikia Mungu na jamii kwa ujumla. Imeanzishwa kwa maono ya wazi ya kuwafundisha wachungaji wenye uzoefu pamoja na wale wanaoingia katika huduma kwa mara ya kwanza. STS inashikilia dhamira ya uaminifu wa kibiblia, usahihi wa mafundisho, na ubora wa huduma katika muktadha wa imani ya Kireformed.

Kwa kujibu hitaji linaloongezeka la viongozi waliofunzwa ambao wanaweza kulitumia Neno la Mungu kwa uaminifu na kutoa uongozi wa kubadilisha jamii zao, STS inatoa programu ya miaka mitatu ya masomo ya theolojia iliyo na mpangilio makini na rahisi kufikiwa. Programu hii inatoa cheti au diploma ya Theolojia na imelenga kuhudumia kundi mchanganyiko la wanafunzi: wachungaji waliowekwa wakfu wanaotafuta msingi zaidi wa kitheolojia, viongozi wa kanisa wanaotamani maandalizi rasmi ya huduma, na wanaoanza wenye shauku ya kufuata wito wa huduma.

STS inatambua kuwa elimu ya theolojia si ya kitaaluma pekee; bali pia ni ya kimaumbile na kimaisha. Hivyo basi, chuo kinachanganya ufundishaji wa kitaaluma wa kiwango cha juu na mazoea ya kiroho yaliyo makusudi, yakiwemo ibada za kila siku, mahusiano ya kimalezi ya kiroho, na maisha ya kijamii yenye uhai. Mtazamo huu wa kina unahakikisha kwamba wahitimu si tu kwamba watapata maarifa ya kitheolojia, bali pia ni watakuwa watu waliokomaa kiroho na wenye hisia za kichungaji.

YALIYOMO

UTANGULIZI....................iii
SALAMU KUTOKA KWA MKUU WA CHUO....................v
1. HISTORIA FUPI YA STS....................1
2. MISINGI YA IMANI....................3
3.VITU VINAVYOTUTOFAUTISHA....................4
4. MUHTASARI WA PROGRAMU....................6
5. WAKUFUNZI....................9
6. MIUNDOMBINU....................11
7. UTHIBITISHO WA ITHIBATI NA FURSA ZA MASOMO....................12
8. MFUMO WA UPIMAJI WA WANAFUNZI....................12
9. KANUNI ZA MAADILI....................14
10. MASHARTI YA KUHITIMU....................15
11. ADA NA MALIPO....................16
12. AMANA YA USALAMA....................18
13. MASHARTI YA UDAHILI....................18
14. JINSI YA KUOMBA....................20
MUHTASARI WA KOZI KWA KILA SEMESTA....................22
SEMESTA YA KWANZA....................22
SEMESTA YA PILI....................22
SEMESTA YA TATU....................23
SEMESTA YA NNE....................24
SEMESTA YA TANO....................24
SEMESTA YA SITA....................25
MSIMBO WA KOZI (COURSE CODES)....................26
Viongozi wa STS....................30

## SALAMU KUTOKA KWA MKUU WA CHUO

Kwa furaha kubwa nakukaribisha katika Chuo cha Theolojia cha Shekinah (STS), taasisi iliyojengwa juu ya msingi thabiti wa Neno la Mungu kwa lengo la kukuza ujuzi wa kitheolojia na moyo wa utume.

Chuo hiki kilianzishwa rasmi tarehe 17 Agosti 2025 kikiwa na msimamo wa dhati wa kufuata kwa uaminifu Maandiko Matakatifu, kushikilia mafundisho safi ya Injili, na kujitoa kwa moyo wote kueneza Habari Njema ya wokovu kwa mataifa yote. Tunatoa elimu ya kiwango cha juu kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza, tukiwapa wanafunzi nafasi ya kukua kielimu, kiroho, na kiutumishi katika mazingira yenye ubora wa kitaaluma.

Ninakuhimiza uwe na amani na furaha unapojifunza katika chuo hiki bora, ukiamini kwamba hapa utapata si tu maarifa, bali pia malezi ya kiroho na msaada utakaoimarisha wito wako. Karibu ujifunze, ujiandae, na uende ulimwenguni ukiwa chombo kilichokamilishwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu.

*“Na mambo yale uliyoyasikia kwangu mbele ya mashahidi wengi, hayo uwakabidhi watu waaminifu watakaofaa kuwafundisha na wengine.” (2 Tim.2:2)*

***Mch. Dkt. Daniel John Seni***
***Mkuu wa Chuo***
***Shekinah Theological Seminary (STS)***

# DIRA

Kuwaandaa watumishi waaminifu wa Kristo kwa ajili ya kutangaza Neno la Halisi, Injili ya Halisi, na kuishi Uhuru wa Halisi uliomo katika Kristo.

# DHIMA

Tupo ili kuwasilisha Injili kupitia elimu thabiti ya kitheolojia, malezi ya kiroho, na mafunzo ya huduma kwa vitendo

# KAULI MBIU

Tukiwa tumetegemea Maandiko, tukitangaza Injili ya Kweli katika Uhuru wa Kristo.

# AHADI YETU

Kusimama katika Maandiko, Kusimama katika Mafundisho ya kweli na Kusimama katika Utume

# 1. HISTORIA FUPI YA STS

Mmisionari. Boyeon Lee kutoka Korea Kusini alitembelea Tanzania kwa mara ya kwanza tarehe 15 Novemba 1995, akifika Kolandoto, Shinyanga. Baada ya ziara hiyo, alirejea nyumbani na mnamo tarehe 18 Aprili 1997 akarudi tena akiwa tayari kwa huduma rasmi ya kimisionari nchini Tanzania. Alifika Mwanza kwa mafunzo ya kimisionari chini ya Africa Inland Mission (AIM), kisha akaenda Musoma kujifunza lugha ya Kiswahili.

Baada ya kupata ujuzi wa Kiswahili, mnamo tarehe 10 Januari 1998, aliwasili Kolandoto kwa ajili ya huduma kama mmisionari chini ya Africa Inland Church Tanzania (AICT). Katika utumishi wake wa kimisionari, Mmisionary Boyeon Lee alitekeleza majukumu yafuatayo: Kwanza, alifundisha katika Chuo cha Biblia cha Kolandoto chini ya AICT; pili, alishirikiana na uongozi wa kanisa kupanda makanisa mbalimbali na kuyaendeleza; na tatu, alianza kozi ya wanafunzi wa kiroho (discipleship) kwa lengo la kuandaa watumishi kwa huduma kubwa zaidi kwa Mungu. Katika kutekeleza jukumu la tatu, alianza kuwaalika na kuwalea vijana wenye wito wa utumishi.

Mwaka 2003, Mmisionary Boyeon Lee alikutana na Daniel John Seni, aliyekuwa mwanafunzi katika Chuo cha Biblia cha Kolandoto katika mwaka wa masomo wa 2003/2004 na baada ya kumaliza masomo yake, Daniel akawa miongoni mwa wanafunzi wake. Mwaka 2006, Mmissionary. Lee akiwa pamoja na vijana wengine (Daniel Seni, Yakobo Jimoku, Eliya Seni) walihamia Dar es Salaam, katika eneo la Mikocheni. Hatimaye, jijini Dar es Salaam, huduma ya wanafunzi wa kiroho ilipewa jina rasmi la Shekinah Mission Centre. Kwa kuwa Shekinah Mission Centre ilikuwa ikiandaa watumishi wa Mungu, kulikuwa na uhitaji wa msingi wa kuanzisha kanisa kama matokeo ya huduma hiyo.

Hivyo basi, mnamo tarehe 13 Mei 2007, ibada rasmi ilifanyika Mikocheni, na kanisa likiwa chini ya Presbyterian Church in Tanzania (PCT). Kwa kuwa Shekinah Mission Centre ndiyo ilikuwa imeanzisha kanisa, ililazimika kutoa jina la kanisa kuwa Shekinah. Haingekuwa busara kuendelea na jina "*Shekinah Mission Centre*" kama jina la kanisa, hivyo likawekwa jina rasmi la Shekinah Presbyterian Church Tanzania (SPCT).

Mnamo tarehe 13 Agosti 2008, Shekinah Mission Centre ilinunua kiwanja kilichopo Madale, Dar es Salaam, kwa ajili ya kuwa kituo cha kudumu cha huduma. Baada ya ununuzi huo, watumishi wa Mungu walianza kukutana katika eneo hilo kila Jumapili jioni kwa maombi. Walikuwa wakikusanyika chini ya mti wa korosho ambao baadaye waliuita AREOPAGO na ambao bado unatumika hadi leo.

Mnamo tarehe 1 Agosti 2010, tulianza rasmi ibada katika eneo la Madale, Dar es Salaam. Tarehe 7.2.2016 Shekinah ilianzisha tawi la kwanza kwa jina la "Shekinah B" na huo ilikuwa mwanzo wa huduma hii kuanzisha matawi.

Kwa hakika, kwa miaka mingi, Shekinah Presbyterian Church, ikiwa chini ya Presbyterian Church in Tanzania, ilikuwa ikipeleka wachungaji wake kusoma katika chuo cha Calvin Theological College.

Kulikuwa na mgogoro wa muda mrefu kati ya Shekinah Presbyterian Church Tanzania na Presbyterian Church in Tanzania, ambapo SPCT ilituhumiwa kuihujumu PCT. Hata hivyo, kikao cha General Assembly cha PCT kilichokaa tarehe 11 Julai 2025 pale Kibamba, CTC, kiliazimia kwamba SPCT ijitegemee na ifanye kazi kama dhehebu kamili linalojitegemea kwani kwa muda mrefu wameendesha shughuli zao bila kuingiliwa. Baada ya uamuzi huo, siku iliyofuata, tarehe 12 Julai 2025, kikao cha kwanza cha SPCT kilikutana Makao Makuu Madale, Dar Es Salaam ili kujadili uamuzi huo. Wachungaji wa SPCT walikubaliana kwa kauli moja kuupokea uamuzi wa PCT, na hivyo wakapitisha rasmi azimio la kuanzishwa kwa chuo kipya cha theolojia chenye jina la Shekinah Theological Seminary (STS).

Shekinah Theological Seminary kiko chini ya usimamizi Shekinah Presbyterian Church Tanzania, lakini kimekusudiwa kupokea wanafunzi kutoka madhehebu mbalimbali nchini Tanzania. Hii inaonyesha dhamira ya chuo kutoa elimu pana na shirikishi, inayolenga kujenga viongozi wenye ujuzi, uadilifu, na moyo wa utumishi, bila kujali tofauti za dhehebu.

## 2. MISINGI YA IMANI

**Shekinah Theological Seminary (STS)** tunaamini mambo yafuatayo muhimu katika Ukristo

### 1. Biblia

Tunaamini kwamba Biblia yote, Agano la Kale na Agano Jipya, ni Neno la Mungu lililovuviwa, lisilo na kosa katika maandiko yake ya awali, na ndilo mamlaka ya mwisho kwa imani na mwenendo. *(2 Tim. 3:16-17; 2 Pet. 1:20-21; Zab. 19:7-9)*

### 2. Mungu

Tunaamini katika Mungu mmoja wa milele anayeishi katika nafsi tatu: Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, walio sawa katika uungu, nguvu, na utukufu. *(Kumb. 6:4; Mt. 28:19; 2 Kor. 13:14)*

### 3. Yesu Kristo

Tunaamini katika Bwana wetu Yesu Kristo, Mungu kamili na Mtu kamili, aliyezaliwa kwa muujiza wa Roho Mtakatifu na Bikira Maria; aliyeishi maisha yasiyo na dhambi, akafa msalabani kama sadaka ya ubadala kwa ajili ya dhambi za wanadamu, akafufuka kwa mwili siku ya tatu, akapaa mbinguni, na atakuja tena kwa utukufu kuwahukumu walio hai na waliokufa. *(Yn. 1:1,14; Lk. 1:34-35; 1 Kor. 15:3-4; Mdo. 1:9-11; Ufu. 22:12)*

### 4. Roho Mtakatifu

Tunaamini katika nafsi na kazi ya Roho Mtakatifu, ambaye huzaliwa upya, hukaa ndani, na huwapa nguvu waamini kwa ajili ya maisha matakatifu, na huwapa karama za kiroho kwa huduma na kwa kujenga Kanisa. *(Yn. 14:16-17,26; Mdo. 1:8; 1 Kor. 12:4-7; Gal. 5:22-23)*

### 5. Mwanadamu

Tunaamini kwamba mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu lakini akaanguka katika dhambi kwa kutotii, hivyo akastahili hukumu ya Mungu. Wokovu unapatikana kwa neema ya Mungu pekee kupitia imani kwa Yesu Kristo pekee. *(Mwa. 1:26-27; Mwa. 3:1-24; Rum. 3:23; Efe.o 2:8-9)*

### 6. Wokovu

Tunaamini kwamba wokovu ni kazi ya neema ya Mungu pekee, iliyokamilishwa kupitia kifo na ufufuo wa Yesu Kristo, na kwamba watu wanahesabiwa haki kwa imani pekee, pasipo matendo ya sheria.*(Yn. 3:16; Rum. 5:8-9; Rum. 10:9-10; Rum. 2:16)*

### 7. Kanisa

Tunaamini kwamba Kanisa ni Mwili wa Kristo, likiwa limeundwa na waamini wa kweli wote. Kanisa limeitwa kumwabudu Mungu, kutangaza Injili, kusherehekea sakramenti, na kuishi kama ushuhuda wa Kristo ulimwenguni. *(Mt. 16:18; Mdo. 2:42-47; Efe. 4:11-13; 1 Kor. 12:27)*

### 8. Kurudi kwa Kristo na Hukumu ya Mwisho

Tunaamini kwamba Yesu Kristo atarudi kwa utukufu kukamilisha mpango Wake wa ukombozi, kufufua wafu, na kuihukumu dunia kwa haki. Waamini watapokea uzima wa milele, ilhali wasioamini watakabili adhabu ya milele. *(Mt. 24:30-31; 1 Thes. 4:16-17; Ufu. 20:11-15; Yn. 5:28-29)*

## 3.VITU VINAVYOTUTOFAUTISHA

Katika Shekinah Theological Seminary (STS), tunaongozwa na misingi maalum inayounda utambulisho, mbinu za ufundishaji, na misheni yetu. Nguzo hizi si tu kwamba zinafafanua sisi ni akina nani kama taasisi ya theolojia, bali pia zinaelekeza aina ya viongozi tunaokusudia kuwaunda kwa ajili ya kanisa na ulimwengu.

**a) Uaminifu wa Kibiblia**

Tunakiri mamlaka ya juu kabisa na ukamilifu wa Maandiko Matakatifu kama Neno la Mungu lililovuviwa. Mafundisho yetu yote, mitaala, na mafunzo ya huduma yamejengwa juu ya mtazamo wa heshima ya juu kwa Maandiko. Tunakusudia kuandaa viongozi wanaoweza kuligawa Neno la kweli kwa usahihi na kulitumia kwa uaminifu katika muktadha mbalimbali ya kichungaji na kitamaduni.

**b) Maono ya Theolojia ya Kireformed**

STS inasimama ndani ya urithi wa kihistoria wa Kireformed Presbyterian, ikikumbatia mafundisho makuu ya neema kama yalivyoelezwa katika Matengenezo ya Kiprotestanti. Wakati tunawakaribisha wanafunzi kutoka madhehebu mbalimbali ya Kikristo, mafundisho yetu ni ya kimaungamo, yakiundwa na utajiri wa theolojia ya Kireformed, ikiwemo mtazamo wa agano, ukuu wa Mungu, na umbo kuu la Kristo katika kila kitu.

**c) Dhamira ya Kimisioni**

Tupo ili kuhudumia misheni ya Mungu duniani. Mafunzo yetu yanawaandaa wanafunzi si tu kwa huduma ya mimbari, bali pia kwa ushiriki wa kina katika uinjilisti, ufuasi wa Kristo, na mageuzi ya kijamii. Iwe katika vijiji vya pembezoni au mijini, wahitimu wetu wamewezeshwa kuhudumu kwa ufanisi na huruma katika wito wao.

**d) Muunganiko wa Kielimu na Kiroho**

STS inathamini nidhamu ya kitaaluma pamoja na malezi ya kina ya kiroho. Wanafunzi wetu wanahimizwa kumpenda Mungu kwa moyo na akili zao. Kupitia masomo ya darasani yenye mpangilio, mazoea ya kiroho yenye nidhamu, na jumuiya hai ya kuabudu, tunalenga kukuza wachungaji na viongozi wanaoishi kwa uadilifu, unyenyekevu, na hekima.

**e) Upatikanaji na Uhusianishaji wa Muktadha**

Mitaala yetu imeundwa ili iweze kufikiwa na wanafunzi kutoka historia mbalimbali za kielimu na huduma. Kwa kutoa masomo kwa Kiingereza na Kiswahili, na kudumisha viwango vya ada vinavyoweza kumudu, tunafanya elimu ya theolojia ipatikane kwa idadi kubwa ya watu. Wakati huohuo, tunahakikisha maudhui yetu yanahusiana moja kwa moja na muktadha wa kanisa la Afrika huku yakibaki na mtazamo wa kimataifa.

## 4. MUHTASARI WA PROGRAMU

Shekinah Theological Seminary (STS) inatoa elimu ya kitheolojia ya miaka mitatu iliyo na mpangilio maalum, iliyoundwa kukidhi mahitaji ya kitaaluma, huduma, na kiroho ya wanafunzi wa aina mbalimbali. Programu hii huishia kwa kutoa aidha Cheti cha Theolojia au Diploma ya Theolojia, kulingana na kiwango cha kujiunga cha mwanafunzi, utendaji wake wa kitaaluma, na kukamilisha kwa mafanikio masharti yote ya kozi.

**a) Muda wa Programu**

Programu kamili imeundwa kukamilishwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu ya masomo, ikijumuisha mihula sita. Kila muhula unatoa ufundishaji wa kina wa masomo makuu ya kiteolojia na ujuzi wa vitendo wa huduma.

**b) Njia za Programu**

- **Cheti cha Theolojia**: Hutolewa kwa wanafunzi wanaokamilisha kwa mafanikio masomo ya msingi ya theolojia, hasa wale wanaoingia wakiwa na historia ndogo ya kitaaluma.

- **Diploma ya Theolojia**: Hutolewa kwa wanafunzi wanaokamilisha programu yote ya kitaaluma kwa matokeo ya kuridhisha na kuonyesha uwezo wa huduma wa kutosha.

**c) Walengwa wa Programu**

Programu ya theolojia ya STS imekusudiwa kuhudumia:

- Wachungaji na viongozi wa kanisa waliowekwa wakfu, wanaohudumu kwa sasa lakini hawana mafunzo rasmi ya theolojia.
- Wanaotarajia kuwa wachungaji au wainjilisti wanaojiandaa kuingia kwenye huduma ya kanisa.
- Wanafunzi wapya wasio na elimu ya awali ya theolojia lakini walio na wito na dhamira ya dhati ya kumtumikia Mungu.

**d) Mbinu za Ufundishaji**

| Kipengele | Maelezo |
|---|---|
| Mbinu za Ufundishaji | Mchanganyiko wa mihadhara darasani, majadiliano ya vikundi, kazi za nyumbani, mafunzo ya huduma ya vitendo, na ulezi wa kiroho. |
| Mfumo wa Kozi | Mtindo wa moduli unaochukua siku nne mfululizo. |
| Idadi ya Vipindi kwa Siku | Vipindi vitano (5) vya masomo na kipindi kimoja (1) cha Chapel. |
| Muda wa Kila Kipindi | Dakika 50 kwa kila kipindi cha masomo na dakika 50 kwa kipindi cha Chapel. |
| Jumla ya Vipindi kwa Kozi | Vipindi 20 vya masomo + Vipindi 4 vya Chapel katika siku nne. |
| Lengo la Mfumo | Kuhakikisha somo linashughulikiwa kwa kina na kuunganishwa na malezi ya kiroho kupitia ibada na maombi ya pamoja. |

**Ratiba ya Kila Simu**

| Saa | Shughuli | Idadi ya Vipindi |
|---|---|---|
| 1:30 – 3:00 | Vipindi viwili | 2 |
| 3:10 – 4:00 | Kipindi cha 3 | 1 |
| 4:00 – 4:30 | Chai | - |
| 4:30 – 6:00 | Vipindi viwili | 2 |
| 6:00 – 6:50 | Chapel | - |
| **Jumla ya Vipindi** | | **5** |

**Kumbuka:** Mitihani, majadiliano, na maswali yatafanyika ndani ya vipindi husika na ni sehemu rasmi ya ufundishaji.

**e) Lugha za Mafundisho**

Masomo hutolewa kwa Kiingereza na Kiswahili, hivyo kufanya elimu ya theolojia ipatikane kwa watu wengi zaidi huku ikilea uwezo wa pande mbili wa lugha za kitheolojia.

**f) Programu za Jioni**

Mbali na programu kuu ya kitaaluma, STS inatoa masomo ya jioni yenye kuandaa wanafunzi kwa ujuzi wa huduma wa vitendo kama vile:

- Stadi za Msingi za Kompyuta kwa Huduma
- Mitandao ya Kijamii na Uinjilisti wa Kidijitali
- Mawasiliano na Uzungumzaji wa Umma

**g) Maendeleo ya Kiroho**

STS ina msisitizo mkubwa juu ya malezi ya kiroho. Wanafunzi wanatakiwa kushiriki katika ibada za kila siku ambapo wanajihusisha na kuabudu, kuomba, kuhubiri, na tafakari za kiroho. Ibada hizi ndizo moyo wa maisha ya kampasi na zinachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa kichungaji na kiroho wa wanafunzi.

### h) Kalenda ya Masomo

Kila muhula unafuata kalenda ya masomo yenye mpangilio maalum, ikiwa na ratiba zilizowekwa wazi kwa ufundishaji, mitihani, na shughuli nyingine za kitaaluma. Masomo hufanyika kuanzia Jumatatu hadi Jumamosi, na huendelea hata katika sikukuu za kitaifa, kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata manufaa ya juu zaidi kutokana na mafunzo yao. Chuo hutoa tarehe zote za kitaaluma mapema ili kurahisisha upangaji wa wanafunzi na walimu na kuwezesha kujitolea kikamilifu katika mchakato wa kujifunza.

### g) Matumizi ya Vitendo

Kadri inavyowezekana, wanafunzi wanahimizwa kutumia wanayojifunza kupitia nafasi za huduma zilizo chini ya usimamizi katika makanisa na jamii za eneo husika. Insha za tafakari, kumbukumbu za huduma, na kazi za uwanjani ni sehemu ya mchakato wa malezi, zikikuza muunganiko wa nadharia na matendo.

## 5. WAKUFUNZI

Nguvu ya Shekinah Theological Seminary (STS) imo kwa kiwango kikubwa katika ubora na upeo wa walimu wake. Wahadhiri wanajumuisha wanaume na wanawake ambao si tu wamehitimu kitaaluma bali pia wamekomaa kiroho na wanashiriki kikamilifu katika huduma za kanisa. Wanaleta darasani utajiri wa uzoefu wa kichungaji, maarifa ya kitaaluma, na moyo wa kujitoa katika kukuza kiroho cha wanafunzi wao.

### a) Sifa za Kielimu
Wafanyakazi wa STS wanashikilia sifa mbalimbali za kitaaluma, zikiwemo:

- Shahada ya Uzamivu (PhD) katika Theolojia, Masomo ya Kibiblia, au fani zinazohusiana
- Shahada za Uzamili (mfano, Master of Divinity, Master of Theology)
- Shahada ya Kwanza katika Theolojia au Huduma ya Kikristo
- Wakufunzi wenye kiwango cha cheti lakini walio na uzoefu mkubwa wa huduma ya vitendo

Mchanganyiko huu wa elimu na uzoefu wa huduma unaiwezesha Seminari kutoa elimu ya theolojia iliyo kamili, inayokidhi viwango vya kimataifa na mahitaji halisi ya huduma za eneo.

**b) Muundo wa Wakufunzi**

STS ina mchanganyiko wa:

- **Walimu wakazi (wa muda wote):** Huwepo kila siku chuoni na hushiriki moja kwa moja katika ufundishaji, ulezi wa kiroho, na majukumu ya kiutawala.

- **Walimu wa kutembelea (wa muda wa sehemu):** Hualikwa kufundisha masomo maalum. Walimu hawa mara nyingi wana uzoefu wa muda mrefu katika huduma ya kichungaji na elimu ya theolojia, wakiwa wamehudumu ndani ya Tanzania na kimataifa. Michango yao huiboresha mazingira ya kitaaluma kwa kuleta mitazamo ya kidunia na maarifa ya vitendo.

**c) Majukumu na Wajibu**

Walimu wa STS hawahusiki tu na kufundisha masomo, bali pia ni walezi wa kiroho na mifano ya kuigwa. Majukumu yao ni pamoja na:

- Kubuni na kufundisha maudhui ya masomo
- Kutoa mwongozo wa kitaaluma na kichungaji
- Kuongoza ibada za chapel na mafundisho ya kiroho
- Kusimamia miradi na kazi za shambani za wanafunzi

- Kuchangia katika malezi ya kiroho na kiteolojia ya wanafunzi

**d) Kujitolea kwa Ubora**

Walimu wetu huchaguliwa si kwa misingi ya mafanikio ya kitaaluma pekee, bali pia kwa maadili yao, unyenyekevu, na shauku kwa misheni ya Mungu. Kupitia mikutano ya mara kwa mara ya walimu, warsha za kuendeleza mitaala, na ushirikiano na mitandao ya kimataifa ya theolojia, STS huhakikisha walimu wake wanabaki na maarifa mapya, wanahusiana na mahitaji ya sasa, na wanafanikisha huduma ya ufundishaji kwa ufanisi.

## 6. MIUNDOMBINU

Shekinah Theological Seminary (STS) imejizatiti katika kutoa mazingira bora, yenye rasilimali za kutosha, yanayowezesha ujifunzaji wa kina wa kitaaluma na malezi ya kiroho. Miundombinu ya seminari imebuniwa kwa umakini ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya wanafunzi na walimu, na hivyo kuruhusu elimu ya theolojia iliyo kamili katika mazingira tulivu na yenye malengo ya kiroho.

STS ina maktaba ya vitabu vya kitheolojia inayokua kwa kasi, ikiwa na mkusanyiko wa vitabu mbalimbali vya Kiingereza na Kiswahili, ikiwemo:

- Biblia na maelezo ya kina ya kibiblia (*commentaries*)
- Vitabu vya theolojia na mafundisho ya imani
- Vitabu vya historia ya kanisa na huduma ya kichungaji
- Maandishi ya kitaaluma, majarida, na rasilimali za kidijitali

Maktaba hii inaunga mkono kazi za masomo ya darasani, utafiti, na kujisomea binafsi, na huendelea kusasishwa ili kuakisi maendeleo ya sasa katika taaluma ya theolojia.

Pia ipo maktaba ya mtandaoni, ambapo mwanafunzi atapata fursa ya kupakua vitabu mbalimbali kwa kadri anavyotaka.

## 7. UTHIBITISHO WA ITHIBATI

Nchini Tanzania, vyuo vya theolojia havisajiliwi chini ya NACTIVET bali huwekwa chini ya usimamizi wa dhehebu kwa dini husika. Shekinah Theological Seminary inafanya kazi chini ya uongozi wa Shekinah Presbyterian Church Tanzania.

Hata hivyo, ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wanaweza kuendelea na masomo ya juu na vyeti vyao vitambulike, tupo katika mchakato wa kusajiliwa na **Accrediting Council for Theological Education in Africa (ACTEA)**. Aidha, kupitia ushirikiano wetu na taasisi mbalimbali, tutawaunganisha na kuwashauri wanafunzi waliohitimu kwa sifa ili waendelee na masomo nje ya nchi.

## 8. MFUMO WA UPIMAJI WA WANAFUNZI

Shekinah Theological Seminary (STS) inatumia mfumo wa kina wa upimaji unaojumuisha tathmini endelevu na mitihani ya mwisho ili kuhakikisha kuwa matokeo ya mwanafunzi yanaonyesha mchakato mzima wa kujifunza na si mtihani wa mwisho pekee.

### a) Vipengele vya Upimaji

Utendaji wa mwanafunzi unahesabiwa kulingana na vipengele vifuatavyo:

- Mahudhurio na Ushiriki Darasani – 10%

- Kazi za Nyumbani na Miradi ya Utafiti – 20%
- Mitihani Midogo na Mitihani ya Katikati ya Muhula – 20%
- Mafunzo ya Vitendo na Ripoti – 10%
- Mtihani wa Mwisho – 40%

**b) Viwango vya Alama na Ufafanuzi**

| Alama (%) | Daraja | Maelezo | Pointi za GPA |
|---|---|---|---|
| 80 – 100 | A | Bora Sana | 4.0 |
| 75 – 79 | B+ | Vizuri Sana | 3.5 |
| 70 – 74 | B | Vizuri | 3.0 |
| 65 – 69 | C+ | Vizuri Kiasi | 2.5 |
| 60 – 64 | C | Wastani | 2.0 |
| 50 – 59 | D | Dhaifu | 1.0 |
| 0 – 49 | F | Amefeli | 0.0 |

**c) Sharti la Kufuzu Somo**

- Mwanafunzi lazima apate angalau alama ya C (60%) ili kufaulu somo lolote.
- Alama ya D au F inamlazimu mwanafunzi kurudia somo na kulipa ada ya marudio kama ilivyoainishwa.

**d) Uhesabuji wa GPA (Grade Point Average)**

GPA inahesabiwa kwa kugawa jumla ya pointi za GPA zilizopatikana kwa jumla ya masomo yote yaliyosomwa. Mfumo huu hutumika kuamua kiwango cha kitaaluma cha mwanafunzi na sifa za kuhitimu.

**e) Viwango vya Kiwango cha Kitaaluma**

- GPA 3.6 – 4.0: Daraja la Kwanza la Heshima (First Class Honours)
- GPA 3.0 – 3.5: Daraja la Pili la Heshima – Sehemu ya Juu (Second Class Honours – Upper Division)
- GPA 2.5 – 2.9: Daraja la Pili la Heshima – Sehemu ya Chini (Second Class Honours – Lower Division)

- GPA 2.0 – 2.4: Amefaulu (Pass)
- Chini ya 2.0: Hastahili Kuhitimu

## 9. KANUNI ZA MAADILI

Shekinah Theological Seminary (STS) imejizatiti kutoa mazingira ya ujifunzaji yenye kumlenga Kristo, yanayodumisha maadili ya kibiblia, uadilifu wa kitaaluma, na heshima ya pande zote. Wanafunzi wote wanatarajiwa kuishi kwa namna inayoakisi tabia ya Kristo na misheni ya Seminari.

**1. Maisha ya Kiroho**

- Wanafunzi watashiriki kikamilifu katika ibada za chapel, maombi, na shughuli nyingine za malezi ya kiroho zinazoandaliwa na Seminari.
- Wanafunzi lazima waonyeshe heshima kwa imani ya Kikristo na kudumisha kanuni za kibiblia katika maneno, matendo, na mwenendo wa maisha.

**2. Uadilifu wa Kitaaluma**

- Kazi zote, tafiti, na mitihani lazima ziwe kazi ya mwanafunzi mwenyewe. Wizi wa kitaaluma (*plagiarism*), udanganyifu, au kutoa taarifa za uongo hairuhusiwi kabisa.
- Wanafunzi wanatarajiwa kuhudhuria madarasa kwa wakati na kutimiza masharti yote ya kitaaluma kwa wakati uliowekwa.

**3. Heshima kwa Wengine**

- Wanafunzi lazima wawatendee walimu, wafanyakazi, wenzao, na wageni kwa heshima, hadhi, na utu kila wakati.
- Uonevu, ubaguzi, au aina yoyote ya unyanyasaji wa maneno, kimwili, au mtandaoni hautavumiliwa.

**4. Mali na Miundombinu**

- Wanafunzi wanapaswa kutunza mali yote ya Seminari, ikiwemo vitabu, vifaa, na majengo.

- Uharibifu wowote unaosababishwa kwa uzembe au makusudi utatozwa kwa mwanafunzi husika.

**5. Mavazi na Mwonekano Binafsi**

- Wanafunzi wanapaswa kuvaa kwa staha na kwa heshima, kwa kuzingatia hadhi ya taasisi ya theolojia.
- Wakati wote wawapo maeneo ya chuo, watalazimika kuvaa sare za chuo.
- Mavazi ya ibada ya chapel na matukio rasmi yanapaswa kuwa ya heshima (formal au semi-formal).

**6. Matumizi ya Vilevi na Vitu Vinginevyo**

- Matumizi au umiliki wa pombe, tumbaku, au dawa za kulevya katika eneo la Seminari ni marufuku kabisa.
- Wanafunzi wanatarajiwa kuepuka mwenendo wowote unaoweza kuharibu sifa ya Seminari.

**7. Hatua za Nidhamu**

- Ukiukaji wa Kanuni hizi za Maadili unaweza kusababisha hatua za kinidhamu, zikiwemo onyo, kusimamishwa, au kufukuzwa, kutegemea uzito wa kosa.
- Seminari inahifadhi haki ya kurekebisha kanuni hizi inapohitajika ili kudumisha mazingira salama, yenye heshima, na yanayomheshimu Mungu.

## 10. MASHARTI YA KUHITIMU

Ili kustahili kuhitimu kutoka Shekinah Theological Seminary, mwanafunzi lazima atimize masharti yafuatayo:

a) Kukamilisha Programu ya Masomo – Mwanafunzi lazima awe amekamilisha kwa mafanikio masomo yote yaliyowekwa kwenye programu yake ya masomo, akipata alama ya kufaulu katika kila somo.

b) Idadi ya Masaa ya Masomo – Mwanafunzi lazima awe amekusanya jumla ya masaa ya masomo (credit hours) yanayohitajika kwa programu ya cheti au diploma.

c) Uaminifu katika Maisha ya Kiroho – Mwanafunzi lazima aonyeshe ushiriki wa kudumu katika maisha ya kiroho ya seminari, ikiwemo:

- Mahudhurio ya ibada za Maombi ya Alfajiri bila kuchelewa.
- Mahudhurio ya ibada zote za chapel (angalau 90%).
- Mahudhurio ya mikutano ya maombi na mikusanyiko mingine ya kiroho iliyo katika ratiba.

**d) Mwenendo Bora** – Mwanafunzi lazima awe na rekodi ya tabia njema na mwenendo wa Kikristo, akionyesha heshima kwa walimu, wanafunzi wenzake, na jamii ya seminari.
**e) Ushiriki katika Huduma ya Vitendo** – Mwanafunzi lazima ashiriki kikamilifu katika huduma na mafunzo ya shambani aliyopewa kama sehemu ya mafunzo yake.
**f) Uhakikisho wa Fedha** – Ada zote za masomo na wajibu wowote wa kifedha kwa seminari lazima ziwe zimeshuluhishwa kikamilifu kabla ya kuhitimu.
**g) Mapendekezo kutoka kwa Walimu** – Mwanafunzi lazima apendekezwe kwa kuhitimu na walimu pamoja na uongozi wa seminari, wakithibitisha kwamba masharti yote ya kitaaluma, kiroho, na kimaadili yametimizwa.

## 11. ADA NA MALIPO

Shekinah Theological Seminary (STS) imejizatiti kufanya elimu bora ya theolojia ipatikane kwa urahisi na kwa gharama nafuu bila kupunguza ubora wa kitaaluma na wa kiroho. Muundo wa ada umeundwa kusaidia wanafunzi kutoka mazingira mbalimbali ya kiuchumi huku ukihakikisha uendelevu wa shughuli za seminari.

### a) Muundo wa Ada

| Aina ya Ada | Kiasi (Tsh) |
|---|---|
| Ada ya Udahili (Mara moja, haina marejesho) | 50,000/= |
| Ada ya Masomo kwa kila Muhula | 300,000/= |
| Kozi ya Jioni (*kwa hiari, kwa kila kozi*) | 100,000/= |

**Kumbuka:** Ada ya udahili inalipwa mara moja tu unapojiunga na haina marejesho. Kozi za jioni ni za hiari lakini zinapendekezwa kwa wanafunzi wanaotaka kukuza ujuzi wa huduma. Mabadiliko yoyote ya ada yatatangazwa mapema.

**b) Sera ya Malipo**

- Ada zote lazima zilipwe kabla au ndani ya wiki mbili za kwanza za kila muhula, isipokuwa kama kumefanywa makubaliano maalum na Ofisi ya Fedha.
- Wanafunzi watakaochelewesha malipo zaidi ya muda wa msamaha wanaweza kuzuiwa kuhudhuria madarasa au kushiriki mitihani.
- Malipo yote lazima yatolewe risiti rasmi na kusajiliwa katika Ofisi ya Hesabu.

**c) Ada Inayojumuisha**

Ada ya masomo inajumuisha:

- Mihadhara na mafunzo yote yaliyo kwenye ratiba
- Ufikiaji wa maktaba na rasilimali za kujifunzia
- Ushiriki katika ibada za chapel na vipindi vya ufuasi
- Mwongozo wa kitaaluma na usimamizi
- Tathmini za ndani na mitihani

**d) Gharama za Ziada (Hazijajumuishwa kwenye Ada)**

Wanafunzi wanashauriwa kupanga bajeti ya gharama zifuatazo ambazo hazijajumuishwa kwenye ada ya masomo:

- Vifaa vya kujisomea na vifaa vya kuandikia
- Safari za huduma au gharama za mafunzo ya shambani (ikiwa zinahitajika)

- Sare rasmi (zinazonunuliwa binafsi na wanafunzi)
- Fulana za michezo na mazoezi ya viungo (wanafunzi wanajibika kununua wenyewe)
- Bima ya afya (mwanafunzi atajihudumia kiafya, lakini ofisi ya chuo itaweza kutoa msaada wa ushauri)

**e) Msaada wa Kifedha na Udhamini**

Ingawa STS haitoi ufadhili kamili wa masomo, msaada wa kifedha mdogo au udhamini wa sehemu ya ada unaweza kupatikana kupitia makanisa ya eneo, wafadhili binafsi, na washirika wa kimataifa. Wanafunzi wanaohitaji msaada wanahimizwa kuwasiliana na Ofisi ya Udahili au Ofisi ya Mkuu wa Taaluma kwa maelezo ya jinsi ya kuomba.

## 12. AMANA YA USALAMA

Kila mwanafunzi mpya anatakiwa kulipa *Amana ya Usalama* mara ya kwanza anaposajiliwa. Amana hii inalenga kuhakikisha uwajibikaji wa mwanafunzi katika kulinda mali, vifaa, na kanuni za seminari.
Kiasi cha amana ya usalama ni TZS 50,000, na lazima kilipwe pamoja na malipo ya kwanza ya ada ya masomo. Amana hii inaweza kurejeshwa mwishoni mwa masomo ya mwanafunzi iwapo:

- Hakuna uharibifu wa mali ya seminari uliosababishwa na mwanafunzi.
- Hakuna ada za masomo au malipo mengine yaliyosalia.
- Mwanafunzi amekamilisha taratibu zote rasmi za kuondoka kabla ya kuacha seminari.

Amana haitarejeshwa endapo mwanafunzi ataacha masomo kabla ya kipindi kilichokubaliwa bila sababu rasmi iliyoidhinishwa na uongozi wa seminari.

## 13. MASHARTI YA UDAHILI

Shekinah Theological Seminary (STS) inawakaribisha waombaji kutoka historia mbalimbali za kielimu, madhehebu, na tamaduni, ambao wanaonyesha wito wa dhati wa huduma ya Kikristo na utayari wa kufundishwa kwa ajili ya utumishi wa uaminifu. Mchakato wetu wa udahili unaongozwa na maandalizi ya kitaaluma pamoja na kujitolea kiroho.

**a) Masharti ya Jumla ya Kujiunga**

Waombaji lazima watimize vigezo vifuatavyo:

- Awe Mkristo aliyeokoka mwenye ushuhuda wa wazi wa imani katika Yesu Kristo.
- Aonyeshe dalili ya wito wa huduma au utumishi wa Kikristo.
- Awe na umri wa angalau miaka 18 wakati wa kuomba.
- Awe tayari kujisalimisha kwa maisha ya kiroho na kitaaluma ya seminari.

**b) Historia ya Kielimu**

- Cheti cha Biblia: Kwa wanafunzi waliomaliza Darasa la Saba (Tanzania).
- Cheti cha Theolojia: Kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne au sawa na hicho, hata bila historia ya awali ya masomo ya theolojia.
- Diploma ya Theolojia: Kwa wanafunzi waliomaliza Kidato cha Sita au wale wenye cheti kinachotambulika cha theolojia kutoka chuo kilichoidhinishwa.

**Kumbuka:** STS pia inapokea waombaji watu wazima ambao huenda hawajakamilisha masomo ya kawaida ya shule lakini wanaweza kuonyesha uzoefu mkubwa wa huduma na ukomavu wa kiroho.

**c) Nyaraka Zinazohitajika**

Waombaji wanapaswa kuwasilisha:

- Fomu iliyokamilishwa ya maombi (inapatikana katika Ofisi ya Udahili).
- Nakala ya kitambulisho cha taifa, kadi ya mpiga kura, au pasipoti.
- Nakala za vyeti vya masomo au vyeti vya kuhitimu shule.
- Picha mbili za pasipoti za hivi karibuni.
- Ushuhuda binafsi wa imani na wito wa huduma.
- Barua ya mapendekezo kutoka kwa mchungaji.
- Nakala ya cheti cha ndoa ikiwa mwombaji ameoa/ameolewa
- Nakala ya cheti cha ubatizo
- Uthibitisho wa malipo ya ada ya udahili (kama ilivyowekwa na seminari).

**d) Usaili na Upimaji**

Kabla ya kudahiliwa, waombaji watashiriki katika mchakato wa tathmini unaojumuisha vipengele vifuatavyo:

- Mtihani wa Kuandika: Kupima kiwango cha ufahamu wa mwombaji kuhusu Biblia.
- Mahojiano: Kubaini wito wa mwombaji kwa huduma, utayari wake wa kusoma masomo ya theolojia, na nia ya kujifunza.

Mchakato huu unalenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaojiunga na Chuo cha Theolojia cha Shekinah wako tayari kielimu na kiroho kwa safari ya masomo na huduma.

## 14. JINSI YA KUOMBA

Wanafunzi watarajiwa wanaokidhi vigezo vya udahili na wanaohisi wito wa mafunzo ya theolojia wanakaribishwa kwa moyo wa upendo kuanza mchakato wa maombi. Shekinah Theological Seminary (STS) imejizatiti kuhakikisha kuwa mchakato huu ni wazi, wa kibinafsi, na unaoongozwa kiroho.

**a) Kupata Fomu ya Maombi**
Fomu za maombi zinapatikana kupitia njia zifuatazo:

- Kwa ana kwa ana katika **Ofisi ya Udahili ya Seminari** iliyopo Mivumoni, Kata ya Wazo, Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam.

- Kwa kuomba kupitia barua pepe: **ststanzania2025@gmail.com**

- Kupitia simu au WhatsApp: **+255 759 883 388**

**Kumbuka:** Fomu hutolewa baada ya kulipa ada ya maombi isiyorejeshwa.

# MUHTASARI WA KOZI KWA KILA SEMESTA

## SEMESTA YA KWANZA

| Na. | Jina la Kozi | Fani ya Masomo |
|---|---|---|
| 1 | Utangulizi wa Biblia | Theolojia ya Kibiblia |
| 2 | Uchunguzi wa Mwanzo | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | Theolojia ya Vitabu vya Musa | Theolojia ya Kibiblia |
| 4 | Muhtasari wa Agano la Kale | Theolojia ya Kibiblia |
| 5 | Muhtasari wa Agano Jipya | Theolojia ya Kibiblia |
| 6 | Kristolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 7 | Utangulizi wa Theolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 8 | Mafundisho Kuhusu Mungu | Theolojia-Pangilifu |
| 9 | Historia ya Mafundisho | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Historia ya Kanisa la Awali | Theolojia ya Kihistoria |
| 11 | Misingi ya Huduma ya Kikristo | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Ufasiri wa Maandiko ya Kikristo | Theolojia ya Kibiblia |
| 13 | Homiletiki | Theolojia ya Vitendo |
| 14 | Theolojia ya Paulo | Theolojia ya Kibiblia |
| 15 | Kanisa la Kiafrika na Mageuzi ya Jamii | Theolojia ya Vitendo |
| 16 | Theolojia Inayohusiana na Muktadha wa Afrika | Theolojia ya Vitendo |

## SEMESTA YA PILI

| Na. | Jina la Kozi | Fani ya Masomo |
|---|---|---|
| 1 | Theodisia ya Kikristo | Theolojia-Pangilifu |
| 2 | Mambo ya Walawi | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | Hesabu | Theolojia ya Kibiblia |
| 4 | Danieli | Theolojia ya Vitendo |
| 5 | Anthropolojia na Harmatolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 6 | Soteriolojia | Theolojia-Pangilifu |

| | | |
|---|---|---|
| 7 | Pneumatolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 8 | Malaika na Mapepo | Theolojia-Pangilifu |
| 9 | Historia ya Kanisa Kipindi cha Kati na Matengenezo | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Historia ya Kanisa la Kisasa | Theolojia ya Kihistoria |
| 11 | Huduma ya Uangalizi na Ushauri | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Uongozi wa Kikristo | Theolojia ya Vitendo |
| 13 | Usimamizi wa Kanisa | Theolojia ya Vitendo |
| 14 | Maadili ya Kikristo katika Muktadha wa Kiafrika | Theolojia ya Vitendo |
| 15 | Kutoka | Theolojia ya Kibiblia |
| 16 | Uinjilisti wa Kisasa na Upandaji Makanisa Afrika | Theolojia ya Vitendo |

**SEMESTA YA TATU**

| **Na.** | **Jina la Kozi** | **Fani ya Masomo** |
|---|---|---|
| 1 | Yoshua na Waamuzi | Theolojia ya Kibiblia |
| 2 | Ruthi na 1 Samweli | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | 2 Samweli na 1 Wafalme | Theolojia ya Kibiblia |
| 4 | 2 Wafalme na 1–2 Mambo ya Nyakati | Theolojia ya Kibiblia |
| 5 | Eklesiolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 6 | Eschatolojia | Theolojia-Pangilifu |
| 7 | Ufafanuzi wa Maungamo ya Imani ya Westminster | Theolojia-Pangilifu |
| 8 | Theolojia ya Agano | Theolojia-Pangilifu |
| 9 | Makanisa Huru ya Kiafrika | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Uinjilisti wa Kimkakati Kupitia Majukwaa ya Kidijitali | Theolojia ya Vitendo |
| 11 | Ibada na Liturujia | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Ukuaji wa Kanisa na Mikakati | Theolojia ya Vitendo |
| 13 | Ulezi na Utengenezaji Wanafunzi | Theolojia ya Vitendo |

| | | |
|---|---|---|
| 14 | Dini na Siasa Afrika | Theolojia ya Vitendo |
| 15 | Uelewa wa Hisia kwa Wachungaji | Theolojia ya Vitendo |
| 16 | Misheni na Uislamu Afrika | Theolojia ya Vitendo |

**SEMESTA YA NNE**

| Na. | Jina la Kozi | Fani ya Masomo |
|---|---|---|
| 1 | Ezra, Nehemia, na Esta | Theolojia ya Kibiblia |
| 2 | Ayubu | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | Zaburi | Theolojia ya Kibiblia |
| 4 | Mithali na Mhubiri | Theolojia ya Kibiblia |
| 5 | Anthropolojia ya Kibiblia | Theolojia-Pangilifu |
| 6 | Theolojia ya Kisasa | Theolojia-Pangilifu |
| 7 | Roho Mtakatifu katika Matendo na Paulo | Theolojia-Pangilifu |
| 8 | Sakramenti na Ibada za Kanisa | Theolojia-Pangilifu |
| 9 | Historia ya Misheni ya Kikristo | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Mijadala ya Kimaafundisho Katika Historia ya Kanisa | Theolojia ya Kihistoria |
| 11 | Ushauri wa Kikristo kwa Ndoa na Familia | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Mbinu Bora za Kufundisha na Kujifunza Kanisani | Theolojia ya Vitendo |
| 13 | Karama za Kiroho na Huduma ya Kanisa | Theolojia ya Vitendo |
| 14 | Yeremia na Ezekieli | Theolojia ya Kibiblia |
| 15 | Kanisa na Maendeleo ya Jamii | Huduma ya Vitendo |
| 16 | Ukristo na Mtazamo wa Dunia wa Kiafrika | Theolojia ya Vitendo |

**SEMESTA YA TANO**

| Na. | Jina la Kozi | Fani ya Masomo |
|---|---|---|
| 1 | Wimbo Ulio Bora na Maombolezo | Theolojia ya Kibiblia |
| 2 | Isaya | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | Utamadunisho na Ibada ya Kiafrika | Theolojia ya Vitendo |
| 4 | Manabii Wadogo | Theolojia ya Kibiblia |

| | | |
|---|---|---|
| 5 | Dini za Ulimwengu | Theolojia ya Kihistoria |
| 6 | Mafundisho Kuhusu Utatu | Theolojia-Pangilifu |
| 7 | Sheria na Injili | Theolojia-Pangilifu |
| 8 | Mazoezi ya Kuhubiri | Theolojia ya Vitendo |
| 9 | Historia ya Kanisa la Kipresbyterian | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Harakati za Uamsho na Upentekoste Katika Historia ya Kanisa | Theolojia ya Kihistoria |
| 11 | Huduma kwa Vijana na Watoto | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Nidhamu na Urejesho wa Kanisa | Theolojia ya Vitendo |
| 13 | Usimamizi wa Sakramenti na Ibada | Theolojia ya Vitendo |
| 14 | Kuinuka kwa Huduma ya Kinabii Afrika | Theolojia ya Vitendo |
| 15 | Wanawake Katika Huduma | Theolojia ya Vitendo |
| 16 | Kanisa na Siasa Katika Jamii ya Kiafrika | Huduma na Masomo ya Muktadha |

**SEMESTA YA SITA**

| **Na.** | **Jina la Kozi** | **Fani ya Masomo** |
|---|---|---|
| 1 | Uchunguzi wa Injili Sambamba | Theolojia ya Kibiblia |
| 2 | Maandiko ya Luka | Theolojia ya Kibiblia |
| 3 | Uandishi wa Kitaaluma Katika Theolojia | Theolojia ya Kibiblia |
| 4 | Waraka za Paulo | Theolojia ya Kibiblia |
| 5 | Kanisa Linalotumia Vikundi Vidogo (CGBC) | Theolojia ya Vitendo |
| 6 | Maandiko ya Yohana | Theolojia ya Kibiblia |
| 7 | Ibada ya Mtandaoni | Theolojia ya Vitendo |
| 8 | Maungamo ya Imani ya Kihistoria | Theolojia-Pangilifu |
| 9 | Mafundisho ya Uongo ya Kihistoria na Kisasa | Theolojia ya Kihistoria |
| 10 | Mifumo ya Uongozi wa Kanisa | Theolojia-Pangilifu |
| 11 | Upandaji Makanisa wa Kistratejia | Theolojia ya Vitendo |
| 12 | Usimamizi wa Migogoro Kanisani | Theolojia ya Vitendo |
| 13 | Masuala ya Kisasa Katika Huduma ya Kichungaji | Theolojia ya Vitendo |

| | | |
|---|---|---|
| 14 | Utetezi wa Imani wa Kisasa wa Kikristo | Theolojia-Pangilifu |
| 15 | Mafunzo ya Huduma ya Vitendo | Theolojia ya Vitendo |
| 16 | Semina ya Huduma na Maandalizi ya Kuwekwa Wakfu | Theolojia ya Vitendo |

**MSIMBO WA KOZI (COURSE CODES)**

# Theolojia ya Kibiblia (BT101–BT130)

| Msimbo wa Kozi | Jina la Kozi |
|---|---|
| BT101 | Utangulizi wa Biblia |
| BT102 | Muhtasari wa Agano la Kale |
| BT103 | Muhtasari wa Agano Jipya |
| BT104 | Uchunguzi wa Mwanzo |
| BT105 | Kutoka |
| BT106 | Theolojia ya Vitabu vya Musa |
| BT107 | Mambo ya Walawi |
| BT108 | Hesabu |
| BT109 | Yoshua na Waamuzi |
| BT110 | Ruthi na 1 Samweli |
| BT111 | 2 Samweli na 1 Wafalme |
| BT112 | 2 Wafalme na 1–2 Mambo ya Nyakati |
| BT113 | Ezra, Nehemia, na Esta |
| BT114 | Ayubu |
| BT115 | Zaburi |
| BT116 | Mithali na Mhubiri |
| BT117 | Wimbo Ulio Bora na Maombolezo |
| BT118 | Isaya |
| BT119 | Yeremia na Ezekieli |
| BT120 | Danieli |
| BT121 | Manabii Wadogo |
| BT122 | Uchunguzi wa Injili Sambamba |
| BT123 | Maandiko ya Luka |
| BT124 | Maandiko ya Yohana |
| BT125 | Waraka za Paulo |

| | |
|---|---|
| BT126 | Uandishi wa Kitaaluma Katika Theolojia |
| BT127 | Ufasiri wa Maandiko ya Kikristo |
| BT128 | Theolojia ya Paulo |
| BT129 | Utangulizi wa Kiebrania cha Kibiblia |
| BT130 | Utangulizi wa Kigiriki cha Agano Jipya |

# Theolojia Pangilifu (ST101–ST120)

| **Msimbo wa Kozi** | **Jina la Kozi** |
|---|---|
| ST101 | Utangulizi wa Theolojia |
| ST102 | Mafundisho Kuhusu Mungu |
| ST103 | Mafundisho Kuhusu Utatu |
| ST104 | Anthropolojia ya Kibiblia |
| ST105 | Anthropolojia na Harmatolojia |
| ST106 | Soteriolojia |
| ST107 | Pneumatolojia |
| ST108 | Malaika na Mapepo |
| ST109 | Kristolojia |
| ST110 | Eklesiolojia |
| ST111 | Sakramenti na Ibada za Kanisa |
| ST112 | Ufafanuzi wa Maungamo ya Imani ya Westminster |
| ST113 | Theolojia ya Agano |
| ST114 | Maungamo ya Imani ya Kihistoria |
| ST115 | Theodisia ya Kikristo |
| ST116 | Eschatolojia |
| ST117 | Sheria na Injili |
| ST118 | Theolojia ya Kisasa |
| ST119 | Mifumo ya Uongozi wa Kanisa |
| ST120 | Utetezi wa Imani wa Kisasa wa Kikristo |

# Theolojia ya Kihistoria (HT101–HT111)

| **Msimbo wa Kozi** | **Jina la Kozi** |
|---|---|
| HT101 | Historia ya Kanisa la Awali |
| HT102 | Historia ya Mafundisho |
| HT103 | Historia ya Kanisa Kipindi cha Kati na Matengenezo |

| | |
|---|---|
| HT104 | Historia ya Kanisa la Kisasa |
| HT105 | Mijadala ya Kimaafundisho Katika Historia ya Kanisa |
| HT106 | Mafundisho ya Uongo ya Kihistoria na Kisasa |
| HT107 | Makanisa Huru ya Kiafrika |
| HT108 | Historia ya Kanisa la Kipresbyterian |
| HT109 | Harakati za Uamsho na Upentekoste Katika Historia ya Kanisa |
| HT110 | Dini za Ulimwengu |
| HT111 | Historia ya Misheni ya Kikristo |

# Theolojia ya Vitendo (PT101–PT133)

| **Msimbo wa Kozi** | **Jina la Kozi** |
|---|---|
| PT101 | Misingi ya Huduma ya Kikristo |
| PT102 | Theolojia Inayohusiana na Muktadha wa Afrika |
| PT103 | Kanisa la Kiafrika na Mageuzi ya Jamii |
| PT104 | Maadili ya Kikristo katika Muktadha wa Kiafrika |
| PT105 | Ukristo na Mtazamo wa Dunia wa Kiafrika |
| PT106 | Ushauri wa Kikristo kwa Ndoa na Familia |
| PT107 | Mbinu Bora za Kufundisha na Kujifunza Kanisani |
| PT108 | Karama za Kiroho na Huduma ya Kanisa |
| PT109 | Huduma kwa Vijana na Watoto |
| PT110 | Nidhamu na Urejesho wa Kanisa |
| PT111 | Usimamizi wa Sakramenti na Ibada |
| PT112 | Mazoezi ya Kuhubiri |
| PT113 | Mafunzo ya Huduma ya Vitendo |
| PT114 | Semina ya Huduma na Maandalizi ya Kuwekwa Wakfu |
| PT115 | Uinjilisti wa Kisasa na Upandaji Makanisa Afrika |
| PT116 | Uinjilisti wa Kimkakati Kupitia Majukwaa ya Kidijitali |
| PT117 | Upandaji Makanisa wa Kistratejia |
| PT118 | Misheni na Uislamu Afrika |
| PT119 | Ukuaji wa Kanisa na Mikakati |
| PT120 | Ulezi na Utengenezaji Wanafunzi |

| | |
|---|---|
| PT121 | Kanisa Linalotumia Vikundi Vidogo (CGBC) |
| PT122 | Ibada na Liturujia |
| PT123 | Ibada ya Mtandaoni |
| PT124 | Utamadunisho na Ibada ya Kiafrika |
| PT125 | Dini na Siasa Afrika |
| PT126 | Kanisa na Siasa Katika Jamii ya Kiafrika |
| PT127 | Kanisa na Maendeleo ya Jamii |
| PT128 | Usimamizi wa Migogoro Kanisani |
| PT129 | Masuala ya Kisasa Katika Huduma ya Kichungaji |
| PT130 | Kuinuka kwa Huduma ya Kinabii Afrika |
| PT131 | Wanawake Katika Huduma |
| PT132 | Uelewa wa Hisia kwa Wachungaji |
| PT133 | Utafiti wa Mwisho wa Huduma |

# Kozi za Hiari (Electives) (EL101–EL105)

| **Msimbo wa Kozi** | **Jina la Kozi** |
|---|---|
| EL101 | Utangulizi wa Kiebrania cha Kibiblia |
| EL102 | Utangulizi wa Kigiriki cha Agano Jipya |
| EL103 | Mitandao ya Kijamii na Ufuasi wa Kidijitali |
| EL104 | Huduma ya Upatanisho na Usuluhishi |
| EL105 | Uponyaji wa Majeraha na Huduma ya Msaada Wakati wa Migogoro |

**Kumbuka:**

- Kozi za hiari zitaanza kutolewa kuanzia mwaka wa pili na kuendelea.
- Hazibadilishi masomo ya msingi bali huongeza upeo wa kielimu na kiutendaji wa mwanafunzi.

# VIONGOZI WA STS

| **Wadhifa** | **Jina** |
|---|---|
| Mkuu wa Chuo | Mch. Dkt. Daniel John Seni |
| Makamu Mkuu wa Chuo | Mch. Ezekiel Kitula |
| Mkuu wa Taaluma | Mwl. Eliya John |
| Mkuu wa Nidhamu | Mch. Japhet Shabani |
| Mkurugenzi Mwanzilishi / Mhasibu Mkuu | Mwl. Boyeon Lee |
| Mkuu wa Huduma za Kiroho (Chaplain) | Mch. Mary Magema |
| Mkuu wa Huduma na Rasilimali | Mch. Benson Makasi |

## WAKUFUNZI WA KWANZA

| **Jina** | **Nyanja** |
|---|---|
| Mwl. Boyeon Lee | Theolojia ya Kibiblia |
| Mch. Yona Amos Isangu | Theolojia ya Kibiblia |
| Mch. Emanuel Nzelah | Theolojia ya Kivitendo |
| Mch. Eliya Tumbegese | Theolojia ya Kibiblia |
| Mch. Dkt. Boazi Park | Theolojia ya Kihistoria |
| Mch. Dkt. Daniel Seni | Theolojia Pangilifu |
| Mch. Ezekiel Kitula | Theolojia ya Kivitendo |
| Mch. Eunice John | Theolojia ya Kivitendo |
| Mch. Elias Subidi | Theolojia Pangilifu |
| Mwl. Eliya John | Theolojia Pangilifu |
| Mch. Japhet Shaban | Theolojia ya Kihistoria |